# MTINDO KATIKA RIWAYA YA *SIKU YA WATENZI WOTE*

**Mussa Mohamed**

*Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

**Ikisiri**

Makala hii inachambua mtindo katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote* kwanza kwa kutoa ufafanuzi wa mitazamo mbalimbali juu ya dhana ya mtindo. Makala inatumia mitazamo jumuishi ya mtindo kama *uteuzi* na mtindo kama *tofauti*. Katika kufanya uchambuzi wa mtindo wa riwaya hii, mhakiki amezama katika vipengele vya matumizi ya uwili, matumizi ya ushairi na matumizi ya vilugha. Vipengele hivi ndivyo ambavyo vinatumiwa na Shaaban Robert kudhihirishia maudhui ya kazi yake ; na umuhimu wa maudhui hayo kwa jamii ya leo unadhihirika hata kama Shaaban Robert aliandika kazi yake zaidi ya miaka hamsini iliyopita.

## Utangulizi

Binadamu huwa na mawazo mbalimbali ambayo hupenda watu wengine wayafahamu. Zipo njia nyingi zinazoweza kutumika kufikisha mawazo hayo kwa jamii au hadhira iliyokusudiwa. Njia hizo za kuwasilishia mawazo ndizo zinazomtofautisha mtunzi mmoja na mwingine na ndizo ambazo baadhi ya wahakiki huziita mtindo. Hivyo twaweza kumtofautisha msanii mmoja na mwingine kulingana na mtindo anaoutumia. Hata hivyo msanii mmoja anaweza kuwa na mitindo zaidi ya mmoja kulingana na aina ya kazi au wazo analotaka kuliwasilisha kwa jamii aliyoikusudia. Shaaban Robert kwa mfano, anaweza kuwa na mtindo wake wa kutunga mashairi, mtindo wa kuandika kazi za nathari na hata mtindo wa uandishi wa barua ambapo mtindo wa kazi moja waweza kuwa tofauti na ule wa kazi nyingine.

Makala hii inakusudia kuchambua mtindo alioutumia Shaaban Robert katika riwaya yake ya *Siku ya Watenzi Wote* kwa kuangalia vipengele mbalimbali vya lugha. Makala pia itajadili maudhui yanayobebwa na vipengele hivyo kwa kuzingatia kuwa mwandishi hakutumia vipengele hivyo kwa kubahatisha tu, bali kuna ujumbe fulani anataka kutufikishia. Hata hivyo licha ya kuwa uchambuzi wa mtindo katika makala hii utajikita katika vipengele vya lugha, si vipengele vyote vya lugha vimechambuliwa bali ni vile tu ambavyo mwandishi wa makala hii ameona vinamtofautisha mtunzi huyu na watunzi wengine au kazi hii na kazi zake nyingine. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, katika kuchambua mtindo wa mtunzi fulani kwa lengo la kumtofautisha na watunzi wengine hatulazimiki kuchambua vipengele vyote vya lugha, bali tunaangalia vile tu vinavyoweza kumtofautisha mtunzi huyo na watunzi wengine. Hii ndiyo kusema kuwa vipengele ambavyo tunaviita kuwa ni vya mtindo wa mtunzi fulani havina budi kumtofautisha mtunzi huyo na watunzi wengine (tazama Crystal, D na D. Davy, 1969 :77). Kwa kuzingatia hoja hii, makala hii itachambua mtindo wa Shaaban Robert katika riwaya teule kwa kuzingatia; matumizi ya uwili, ushairi na vilugha.

Kabla ya kuanza kufanya uchambuzi, ni vizuri tukaanza kwa kujadili dhana ya mtindo. Mtindo si dhana ngeni hasa ukizingatia kuwa unamuhusu binadamu na

maisha yake ya kila siku. Hivyo basi, ni jambo la kawaida kusikia mtu anamtathmini mtu mwingine kwa kusema mtindo wake unavutia au mtindo wake si mzuri. Wataalamu mbalimbali wamejadili dhana ya mtindo kwa mitazamo tofauti.

Gray (1969) kama alivyonukuliwa na Enkvist (1973) anauona mtindo kama nguo au vazi ambalo lipo kwa kuwa tu watu wanataka kuliona kama ilivyo mazoea. Hoja ya msingi hapa ni kuwa mtindo ni kitu kinachoweza kuwepo au kutokuwepo. Unakuwepo tu pale unapohitajika. Katika hali ya kawaida tumezoea kuwaona watu wakiwa wamevaa nguo, japo pia kutokuvaa nguo haina maana kuwa zile sifa za msingi za kumfanya mtu huyu aitwe mtu hazitakuwepo.

Tofauti na Gray, Enkvist (1973) anasema kuwa mitazamo yote ya kiisimu kuhusu mtindo inaweza kujikita katika moja kati ya mitazamo mikuu mitatu. Kwanza, mtindo ni **ukiushi** wa kaida zilizowekwa au zilizopo. Kwa mujibu wa mtazamo huu, uchambuzi wa mtindo hufanywa kwa kulinganisha nduni zilizo katika matini inayoshughulikiwa na zile ambazo zitarejelewa kama kaida. Kama kwa mfano, ushairi wa kimapokeo sharti uzingatie urari wa vina na mizani, pakawa na mtunzi atakayeandika ushairi wake wa kimapokeo bila kuzingatia kipengele hicho, huo utakuwa ni mtindo wa mtunzi huyo.

Pili, mtindo unatazamwa kama **nyongeza.** Kwa mujibu wa mtazamo huu, katika utunzi wa kazi yeyote huwa tunakuwa na vipengele vya msingi ambavyo ndivyo vitaifanya kazi hiyo iwe na hadhi fulani. Mathalani, katika uandishi wa riwaya, kama tukiambiwa sharti iwe na maneno elfu kumi (huu ni mfano wangu), akatokea mtunzi fulani na kuandika riwaya yenye idadi hiyo ya maneno ila akaamua pia kuongeza idadi ya maneno kwa kutumia mbinu mbalimbali kama mashairi au/ na nyimbo ndani ya riwaya, huo utakuwa ni mtindo wa mtunzi huyo.

Tatu, mtindo unatazamwa kama **kidokezo** ambapo nduni mbalimbali za kiisimu kama zilivyotumika katika matini zinahusishwa na mazingira halisi ya jamii. Hivyo basi, uchambuzi wa mtindo kwa kuzingatia mtazamo huu unalenga kuangalia uhusiano uliopo baina ya vipengele mbalimbali vya kiisimu na mazingira halisi ambamo vipengele hivyo vinatumika. Mathalani, matumizi ya lugha zisizo rasmi yanaweza kumbainisha mhusika fulani na mahali au / na tabaka alilotoka.

Hata hivyo licha ya kuwa na mitazamo hiyo mitatu kuhusu mtindo, mitazamo hiyo hutegemeana na kukamilishana. Hakuna mtazamo ambao wenyewe tu ndiyo utakaotumika katika mazingira yote. Kuna wakati ambapo mtazamo wa mtindo unaweza kuonekana kuwa ni ukiushi, wakati mwingine ukaangaliwa kama nyongeza na wakati mwingine tukalazimika kuuangalia mtindo kama kidokezo. Mitazamo hii yaweza tu kutofautiana kimatumizi kwa kutegemeana na aina za matini.

Kahigi (1997) kwa kufuata nyayo za wataalamu waliotangulia, wakiwemo G Leech na M. Short (1981), ameangalia mtindo katika mitazamo miwili. Mtindo kama uteuzi na mtindo kama tofauti. *Mtindo kama uteuzi* husisitiza kuwa mzungumzaji au mwandishi huteua vipengele maalum miongoni mwa vipengele vilivyomo katika lugha husika na kivitumia katika kazi zao. Ni kwa kutumia mtazamo huu ndipo tunapoweza kubaini tofauti iliyopo baina ya lugha na mtindo; kuwa lugha ni jumla ya vipengele vyote anavyoweza kuvitumia mzungumzaji au mwandishi katika kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa, wakati mtindo ni vile vipengele vichache tu atakavyoviteua katika muktadha maalum. Mtazamo huu unaungana na mawazo ya Crystal na Davy (1969:77) pale waliposisitiza kuwa, uchambuzi wa mtindo hauwezi kufanywa kwa kuzingatia vipengele vyote vya lugha kwani lugha ni pana zaidi na mtindo ni sehemu tu ya matumizi ya lugha. Hivyo basi uchambuzi wa mtindo unatakiwa ujikite tu katika vile vipengele ambavyo vitamtofautisha msanii huyo na wasanii wengine.

*Mtindo kama tofauti* unachukuliwa kama ni yale mambo yanayovitofautisha vipengele vya lugha vilivyotumiwa katika kazi fulani na kaida zilizopo. Hapa tunazingatia ukweli kuwa kila uwanja una kaida zake. Mathalani zipo kaida za uandishi wa mashairi, riwaya, barua na nyingine nyingi. Hivyo tunapochambua mtindo kwa kuzingatia mtazamo huu tunaangalia tofauti ya vipengele vya lugha iliyopo baina ya kazi tunayoishulikia na kaida za kiisimu zilizopo. Kama, kwa mfano, katika kaida iliyopo ya uandishi wa barua za kikazi anwani ya mwandishi inakuwa upande wa kulia na ya mwandikiwa inakuwa upande wa kushoto, akatokea mtaalamu na kufanya kinyume chake, huo utakuwa ni mtindo wake. Mtazamo huu unafanana na ule wa Enkvist (ameshatajwa) unaouona mtindo kama ukiushi, kwa kuwa pamoja na kuwa mtunzi wa aina hii anafanya kitu ambacho ni tofauti na wengine, lakini pia anakiuka kaida zilizopo.

Hata hivyo, pamoja na juhudi za mtaalamu huyu za kuiweka mitazamo mbalimbali katika makundi makuu mawili, bado kuna mwingiliano mkubwa baina ya mtazamo unaouona mtindo kama uteuzi na ule unaouona mtindo kama tofauti. Tukiangalia hoja ya Crystal na Davy kwa mfano, inayosisitiza kuwa uchambuzi wa mtindo unatakiwa kulenga tu vipengele ambavyo vinamtofautisha mtunzi mmoja na mwingine, tunaona kuwa mitazamo yote miwili inaingia hapa. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, mtunzi yeyote anapoandaa kazi yake hulazimika kuteua vipengele fulani mahususi ili kufikisha ujumbe wake. Wakati huo huo, mtunzi huyu anaweza kutofautiana na watunzi wengine kwa kutumia vipengele hivyo ambavyo watunzi hao watakuwa hawajavitumia katika kazi zao. Hivyo basi ni wazi kuwa dhana ya mtindo bado ni bahari pana yenye kina kirefu inayomruhusu kila mwenye ujuzi wa kuogelea kufanya hivyo na hatimaye kuibuka na mitazamo mingine mingi inayofafanua dhana hii.

Kwa kuwa ipo mitazamo mingi inayohusu dhana ya mtindo, makala hii itajikita katika mitazamo miwili ya mwisho iliyofafanuliwa hapo juu, yaani mtindo kama **uteuzi** na mtindo kama **tofauti.** Hii ni kutokana na ukweli kuwa mitazamo hii miwili haina mipaka mahususi, hivyo nayo pia inaingiliana na kukamilishana.

**Matumizi ya uwili**

Kuna baadhi ya maneno ambayo tumezoea yanapotumika huenda pamoja, kwamba moja likitumika tunajenga fikira kuwa kuna jingine, wengine huweza kuyaita maneno tangamano. Maneno haya yanaweza kutumika kusisitiza mambo mbalimbali, miongoni mwa mambo hayo ni umoja na mshikamano. Pamoja na ukweli kuwa katika jamii yetu zipo dini mbalimbali, Shaaban Robert katika *Siku ya Watenzi Wote* anaonesha kuwa kwa sehemu kubwa wanajamii wamegawanyika katika imani za dini ya Uislamu au Ukristo, na anasema kuwa tukifanikiwa kuunganisha watu hawa basi tutakuwa tumeiunganisha sehemu kubwa ya jamii yetu. Kwa kutumia dhana ya uwili mwandishi kwa sehemu kubwa amekuwa akitaja Msikiti na Kanisa kuonesha kuwa jamii yetu imeharibika licha ya kuwa wengi wanajiita ni waumini wa Ukristo au Uislamu. "*Huwa namna ya onyesho la mema machache; na maovu mengi yaliyoenea kwa kujificha katika kila pahali, hata katika milango ya Misikiti na Makanisa*." (Uk.46) Hapa mwandishi anatuonesha kuwa wapo watu ambao wamekuwa wakitumia mgongo wa dini katika kufanya mambo ambayo ni kinyume na maadili ya jamii zetu.

Hata hivyo, Shaaban Robert anaendelea kututanabahisha kuwa hapo awali Misikiti na Makanisa palikuwa mahali pasafi tena palipotegemewa na watu walio wengi ambapo hapakuwa na tofauti kati ya masikini na tajiri kwani watu walitoa zaka zao ambazo ziliwasaidia wasiokuwa na uwezo. Tatizo linakuja pale ambapo amri ya Mwenyezi Mungu imesahauliwa na kuwa watu wanaishi maisha ya dhiki na tabu nyingi. Anasema :

> Zamani kwa kweli Kanisa au Msikiti ulikuwa safi, na kwamba kwa sababu ya kusahau wajibu wake safi, ulijitatiza wenyewe na mambo ya dunia hii, hata kazi yake ikawa haifai kabisa na kwamba ndipo dunia ilipokuwa imetumbukia katika hali yake ya sasa ya upotovu na maangamizi. Kwa kweli laiti pangelipatikana Msikiti au Kanisa lililo safi, na lililo katika utii wa amri za Mungu, lenye kupokea ushuria ya ziada ya ulimwengu, mashaka yasumbuayo wanadamu lazima yangalitatuliwa mara moja au yasingalikuwepo" (uk.47)

Hapa mwandishi anatumia Msikiti na Kanisa kuonesha namna taasisi hizi zilivyopoteza mwelekeo na malengo ya kuanzishwa kwake. Hata hivyo anamalizia kwa kusema kuwa kama taasisi hizi zingetimiza wajibu wake hali isingekuwa kama hivi ilivyo.

Hivyo basi, kwa sehemu kubwa mwandishi amezingatia matumizi ya uwili katika kuonesha umuhimu wa kuwa na dini ya umoja ambayo itajumuisha dini kuu mbili yaani Uislamu na Ukristo. Anasisitiza kuwa, kwa kuwa tumeweza kuwa na umoja wa aina mbalimbali mathalani, Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika, kuna uwezekanao pia wa kuwa na umoja wa dini. Haya yanadhihirishwa na Adili pale alipoulizwa na Sara kama suala la kuwa na dini ya pamoja katika jumuiya ya Adili ni suala linalowezekana.

> Sioni kuwa shida. Jumuiya imekwisha jithibitisha yenyewe kuwa bora kwa kufuata mwenendo wa ulimwengu na tabia ya watu wake. Pana umoja wa mataifa, pana umoja wa dola, pana umoja wa rangi, pana umoja wa udugu kwa ajili ya manufaa ya maisha ya

> kitambo. Si ajabu kukosekana umoja wa dini kama ulimwengu wataka kweli kuendesha na kutimiza wajibu wake?........... (uk.83)

Kwa kuonesha msisitizo juu ya suala hili la umoja wa dini, mwandishi anawataja sana viongozi wa dini kuu mbili na sehemu zao za ibada. Mathalani, kila alipomtaja Sheikh amemtaja pia Padiri, kila alipotaja Msikiti, ametaja pia Kanisa, vivyo hivyo pale mwandishi alipotaja vita ya Msalaba, ametaja pia Jihadi. Jambo hili linatufanya kuona upekee wa mwandishi huyu hasa katika matumizi ya uwili ambapo dhana na umuhimu wa kuwa na umoja wa dini imejadiliwa kwa upana zaidi. Hata hivyo, licha ya kuwa mwandishi anazungumzia suala la umoja wa dini, suala hili linaweza kuangaliwa kwa mapana zaidi, mathalani umoja katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Umoja katika nchi za Afrika Mashariki na kadhalika.

Kutokana na marudio ya mara kwa mara ya maneno haya yenye uwili tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa huu pia ni mchomozo wa mwandishi huyu ambao kwa hakika haujatokea tu kwa bahati mbaya bali kuna jambo zito ambalo mwandishi alitaka hadhira ilifahamu, nalo ni suala la umoja na mshikamano bila kuzingatia tofauti ya dini zetu. Hali hii inatupa picha ya namna mwandishi huyu alivyokuwa na upeo wa kuona mbali, kwani yeye aliona kuwa kitu ambacho kinaweza kuhatarisha umoja wetu kwa kiasi kikubwa ni imani ya dini ambayo kwa sehemu kubwa ndiyo inayoweza kuigawanya jamii katika makundi mawili kama ilivyokuwa kwa watu wa Rwanda na Burundi ambao umoja wao ulihatarishwa na makabila kutokana na kuwa na makabila makuu mawili yaani Wahutu na Watusi. Umoja anaouzungumzia mwandishi wa riwaya hii, ndiyo ule ambao leo hii viongozi wa dini wanaumiza vichwa vyao kuona uwezekano wa kuwa na umoja ambao hautaegemea katika dini yeyote. Hii imepelekea viongozi wa dini ya Kiislamu na Kikristo kukutana mara kwa mara na kuangalia namna ya kujenga na kuimarisha umoja huu. Katika harakati za kufikia lengo lao hili, viongozi hawa walifikia hata hatua ya kupendekeza kuwa na mtaala mmoja wa kufundishia somo la dini katika shule za msingi.

Kutokana na ukweli kuwa maendeleo ya kweli hayawezi kufikiwa bila jamii zetu kuwa na umoja wa dhati, dhana ya umoja imekuwa ikijadiliwa katika kazi mbalimbali, ziwe za kifasihi au zisizo za kifasihi. Ndiyo maana tuna Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na Umoja wa nchi zilizo kusini mwa jangwa la Sahara na kadhalika. Waandishi wa kazi za fasihi nao hawakuwa nyuma katika kulijadili suala hili. Wamekuwa wakilieleza kulingana na aina ya jamii inayozungumziwa. Wapo walioeleza umoja kwa kuzingatia matabaka yaliyopo, wengine wamezingatia umri na wengine wamezingatia makabila. Katika jamii ya watu wa Rwanda kwa mfano huwezi kuzungumzia suala la umoja ukakwepa kutaja Wahutu na Watusi, kwani watu hawa hutofautiana kwa kuzingatia tofauti za makabila yao.

Shaaban Robert kwa upande wake, ilivyoelezwa hapo juu, amelijadili suala la umoja kwa kuzingatia tofauti za kidini. Mwandishi anaona kuwa hali mbaya ya maisha tuliyo nayo inatokana na viongozi wa dini kushindwa kutekeleza wajibu

wao. Haya anayaeleza kupitia kwa mhusika wake Ayubu ambaye anajulikana kama Hatibu wa Jumuiya ya Adili. Ayubu amekuja na mtazamo kuwa dini za kigeni (Uislamu na Ukristo) zimekuwa zikiwapa wafuasi wake mafundisho ambayo yamkini yamekuwa yakiwaacha njia panda. Haya yanathibitishwa na maneno yake pale aliposema "Tunajaribu kufundisha watu wetu kutazama ng'ambo ya msalaba na jihadi. Twafikiri kwamba hapa ndipo Kanisa na Msikiti viliposhindwa. Huwapeleka watu katika Msalaba na Jihadi vikawaacha huko. Twataka kuwachukua mbele, katika uzima wao hata katika ufufuo. (uk.11-12).

Hapa mwandishi anatuonesha kuwa kuna umuhimu wa kuachana na imani ya dini za kigeni na kuunda dini ya umoja ambayo ndiyo itakayokuwa suluhisho la matatizo tuliyonayo. Jambo la msingi la kujifunza hapa ni kuwa, licha ya kuwa mwandishi anaamini viongozi wa dini ndiyo chanzo cha matatizo tuliyo nayo, bado anasisitiza kuwa suluhu iliyopo ni wanajamii wa dini hizi kuungana na kuunda umoja wa dini.

Ikumbukwe pia kuwa Shaaban Robert aliandika riwaya hii katika kipindi ambacho nchi ilikuwa inaelekea kujitawala baada ya kutoka kwenye makucha ya kutawaliwa kwa miaka mingi. Hivyo basi ni wazi kuwa mwandishi huyu alikuwa anatoa nasaha kwa viongozi watakaokuwa madarakani kuhakikisha kuwa suala la umoja miongoni mwa wanajamii linapewa kipaumbele. Jumuiya ya Adili huenda ndiyo nchi ya Tanzania (Tanganyika ya wakati huo) ambayo baada ya kupata uhuru wake, ilitegemewa kuwa kutakuwa na uhuru wa kujieleza na ugawanyaji mzuri wa rasilimali za nchi ambazo mwandishi huyu aliziita zaka. Hivi sasa tunasikia malumbano yanayoendelea dhidi ya watu wanaoitwa mafisadi kwa vile waliamua kujilimbikizia mali ambazo kimsingi zilitakiwa zitumike kwa maslahi ya umma wote wa Watanzania.

Zaidi ya kutumia dhana ya uwili katika kuonesha umuhimu wa kuwa na umoja wa dini, mwandishi pia ametumia dhana hii katika maneno mengine kama, watoto na watu wazima (uk.14), wanaume na wanawake (uk.30), Kiswahili na Kiingereza (uk.30), kuchukua na kuacha (uk.32), mashariki na magharibi (uk.62), waganga na wachawi (uk.81) na mengine mengi.

**Matumizi ya ushairi**

Matumizi ya ushairi pia ni mbinu mojawapo ambayo mwandishi anaweza kuitumia katika kufikisha ujumbe wake kwa hadhira aliyoikusudia. Ushairi huweza kuwa ni mbinu ambayo hutumiwa zaidi pale msanii anapokuwa na jambo zito analotaka kulifikisha kwa hadhira iliyokusudiwa. Shaaban Robert ni miongoni mwa watunzi mashuhuri wa ushairi wa Kiswahili. Kabla ya kufariki dunia alikuwa amefanikiwa kuandika kazi mbalimbali za ushairi, miongoni mwa kazi hizo ni *Almasi za Afrika, Pambo la lugha, Ashiki kitabu hiki* na nyingine nyingi.

Katika riwaya hii, mwandishi pia ametumia ushairi kila alipotaka kusisitiza jambo ambalo anaamini ni muhimu hadhira ilielewe kwa undani zaidi. Mwandishi

anaanza kutumia shairi kwa kutuonesha kuwa katika jamii yetu wapo watu wanaojiita viongozi wa dini na pengine hata viongozi wa siasa ambao wanapokuwa katika mfumo wa uongozi huwa washabiki wa kusifu mfumo wa uongozi uliopo. Hata hivyo mara watu hawa wanapokuwa nje ya uongozi, ama kwa kumaliza muda wao ama kwa kuachishwa huanza kuukejeli mfumo uliopo na kuona kuwa hauna maana. Anasisitiza hili pale aliposema, watu hawa wakiwa madarakani husema;

*Kichaka hiki kizuri,*
*Kwa marashi na uturi,*
*Harufu yake si nzito,*
*Kwa tamu ya manukato*. ( uk.7)

Watu hawa wanapokuwa nje ya madaraka yao hubadilisha lugha na kulalama:

*Kichaka hiki kichafu,*
*Kwa uvundo wa harufu,*
*Ya gugumo na kutizi,*
*Na ubaya wa pumzi*. (uk.7)

Japo mwandishi aliyasimulia mambo haya miaka mingi iliyopita kwa sasa ndiyo yanaelekea kushamiri katika jamii. Ni jambo la kawaida kuwaona watu walio kwenye madaraka na wakashabikia mfumo uliopo hata kama ni mbovu. Hata hivyo watu hao wanapokuwa nje ya madaraka huanza kutoa hoja mbalimbali wakilaumu wenzao waliowaacha katika madaraka. Tunashuhudia wanasiasa wengi wanaoamua kujiunga na upinzani na kuanza kukebehi mfumo uliopo utadhani kuwa wao hawakuwa katika nafasi hizo muda mchache uliopita. Kwa upande wa viongozi wa dini, hali siyo tofauti ambapo tunashuhudia wimbi la viongozi wa dini wanaolumbana wao kwa wao na wakati mwingine baina yao na viongozi au waumini wa dini nyingine. Ndio maana hatuishi kusikia kuhusu migogoro katika makanisa na misikiti inayotangazwa mara kwa mara kwenye vyombo vya habari vya ndani na nje ya nchi.

Vilevile mwandishi anatuonesha kuwa katika jamii yetu, kuna watu ambao wanajificha katika mgongo wa dini na kujifanya ni waumini safi, lakini watu hao kwa hakika ni wadhulumaji wakubwa ambao pia wanaendesha biashara haramu kama vile kuwa na madanguro na maghala ya bangi.

*Wa angani*
*Ndiyo ndege warukao,*
*Wenye dini*
*Ndiyo nyoka waumao* (uk.27)

Hapa mwandishi anasisitiza kuwa wale walio katika madaraka ndiyo chanzo cha matatizo na kuwa wao ndio wanaokula jasho la wanyonge na kuwa wale wanaojiita wenye dini ndiyo maadui wa haki za wananchi.

Mwandishi pia amemtumia mhusika wake Sarah kuonesha namna ambavyo watu ambao wanadhaniwa kuwa ndiyo mfano wa kuigwa kwa kuwa wao ni viongozi wetu, wanavyokuwa vinara wa kutenda makosa. Mwandishi anasisitiza,

*Watu wenye utukufu katika dunia hii,*
*Ndiyo wawao dhaifu, fahamu kama hujui,*
*Na wenye utakatifu na maarifa na rai,*
*Ndiyo walao nyamafu na wakuu wa jinai* (uk.76)

Ni jambo la kawaida katika jamii yetu tuliyo nayo sasa kusikia viongozi wa dini ambao ndio tuliwategemea wawe watukufu wanaowawakilisha manabii, kuwaona wanatenda mambo machafu kama ubakaji, wizi, ushirikina na mengine mengi. Hivyo basi, licha ya kuwa mwandishi aliandika kazi hii miaka mingi iliyopita, mafundisho yake bado yangali yanafanya kazi katika jamii yetu, hasa katika zama hizi zijulikanazo kuwa ni za utandawazi - yaani dunia kuwa kama kijiji kimoja.

Kadhalika mwandishi ameendelea kutumia mtindo wa mashairi katika kusisitiza umuhimu wa maadili mema na kuwa utukufu au ubora wa mtu hutokana na maamuzi yake muumba. Kwa maana kuwa akili na upeo wetu ni mdogo sana katika kung'amua mambo mbalimbali, isipokuwa Mungu muumba ndiye huamua ni nani wa kumpa uwezo wa kujua mambo ambayo yapo nje ya uwezo wa akili zetu. Mwandishi anasema;

*Dunia hutazama watu kata mahiri akili,*
*Dunia kama msitu inatatiza kwa feli*
*Lakini Muumba wetu, Msanifu wa adili,*
*Huipa roho ya mtu kujua yasiyo ya mwili.* (uk.88)

Mwandishi analidhihirisha hili kupitia kwa muhusika wake Zakaria ambaye anaonekana kujaaliwa hekima na busara toka kwa Mungu. Kwa hakika, Mwandishi huyu ni miongoni mwa watu wenye mtazamo kuwa uwezo na upeo wa mtu katika sanaa, vinatoka kwa Mungu na wala si juhudi binafsi. Zakaria kwa kutumia hekima zake aliweza kumshawishi Sarah kufuta hasira na chuki aliyokuwa nayo dhidi ya Izak. Katika shairi hili tunaweza kubaini msimamo wa mwandishi juu uwepo wa Mungu na nafasi yake katika maisha yetu ya kila siku.

Mwandishi pia amemalizia masimulizi yake kwa shairi kuwa haya yote aliyoyasimulia yapaswa pia kutumika kama kumbukumbu yake kwa vizazi vijavyo. Huu ni upeo wa kipekee kwa mwanadamu kuweza hata kutabiri juu ya maisha yake na siku zake za kuishi hapa duniani. Katika ubeti huu, mwandishi anasema;

*Tamati natia mwisho kuwahadithia shani,*
*Hadithi ya furahisho kwa jamii duniani,*
*Kuwa kama makumbusho ya mtunzi Shaaban*. (uk.106)

Katika ubeti huu pia mwandishi anatukumbusha, pamoja na mambo mengine, umuhimu wa kuacha wasia ambao utawanufaisha wale utakaowaacha duniani.

Wasia ninaoukusudia hapa hasa ni ule wa fikra na mawazo kwani wapo wataalamu wengi sana ambao wamekuwa wakiaga dunia siku baada ya siku bila hata kuacha athari za kitaaluma ili kizazi kinachobakia kiweze kuyafaidi yale waliyonayo wataalamu hawa kwa faida ya kizazi cha sasa na hata cha baadaye. Mwandishi aliishi kipindi kifupi sana baada ya kuandika riwaya hii iliyoandikwa kwa mtindo wa kipekee, ambapo mwandishi amehakikisha kuwa anatumia mbinu mbalimbali kufikisha ujumbe alioukusudia kwa hadhira husika.

Jambo la kipekee pia ambalo mwandishi wa riwaya hii amelionesha ni namna alivyoanza masimulizi yake ambapo ameanza na kibwagizo cha Paukwa Pakawa, na hatimaye kumalizia kwa ubeti wa ushairi. Haya yanatuonesha mtindo wa kipekee aliokuwa nao mwandishi huyu katika uandishi wa kazi za fasihi hata yakamfanya mwandishi wa makala hii kuona kuwa huu ni mtindo wa Shaaban Robert ambao unaweza kumtofautisha na waandishi wengine wa riwaya ya Kiswahili hasa ikizingatiwa wakati alipoiandika riwaya yake.

**Matumizi ya vilugha**

Hii ni mbinu nyingine ambayo mwandishi wa riwaya hii ameitumia katika kufikisha ujumbe wake kwa hadhira husika. Vilugha hapa ina maana ya lugha ambayo kimuonekanao ni kama Kiswahili lakini inawakilisha watu wa kundi fulani. Wengine wangeweza kuona kama ni lahaja, lakini mwandishi wa makala hii hakuona sababu ya kufanya hivyo kwa kuwa hana ushahidi wa kiisimu kuthibitisha juu ya hoja hiyo. Lengo la kutumia vilugha ni kumfanya msomaji abaini aina ya mhusika anayezungumziwa na lugha anayoitumia. Kutokana na vilugha msomaji anaweza kubaini kuwa ama mhusika huyu ni mtoto, mtu wa mashamba, mtu asiyejua vema Kiswahili kutokana na asili yake n.k. Matumizi ya vilugha kwa kawaida huvilenga vikundi maalum katika jamii kama vilivyotolewa mfano hapo juu.

Mwandishi anamtumia mhusika wake Ayubu, pale alipotembelea katika mtaa ambao wakazi wake wengi ni watu wa hali ya chini kutokana na vipato vyao vidogo katika kazi zao za kila siku. Ayubu baada ya kufika katika mtaa huu anakutana na watoto wawili wadogo. Wale watoto baada ya kumuona Ayubu walifurahi sana, hali iliyoashiria kuwa walikuwa na taarifa njema za mtu huyu. Watu wengi wanaoishi katika mtaa huu, wakiwemo watoto wale, wanamfananisha na malaika au mkombozi wao kutokana na moyo wa ukarimu alio nao.

Anapowauliza kuwa nani kawaambia juu ya habari zile yule mtoto anasema, "*Bi Lela bwana. Yeye hufagia kitalu cha Jumuiya ya Adili kila 'lasiri katika Jumamosi. Lali na mie 'saidia ye chukua kapu 'ake pengine; nasi 'ingia ndani wakati wa hotuba ku 'ingine. Sisi jua kuwa we ndiye hatibu 'kuu watu 'ingine ita we 'laika*... (uk.28)

Wakati walipokuwa wanaendelea na mazungumzo, mara kwa mbali akaonekana mwanamke mmoja ambaye inasadikiwa kuwa alinyimwa ujira wake kwa

kuambiwa eti alifanya tafsiri mbovu kwa kuwa alikuwa ametumia maneno ya kigeni kwa wingi zaidi. Yule mtoto akaonyesha kwa kidole chake barabarani na kusema, "*Yule kwenda Bi Nunu na 'koba 'ake. Kama fukuzwa kazini 'taabika. Watu sema kama hivi. Tajiri 'ake 'kalia ye na 'guu kausha-kwa 'ovu. Mpa ye 'akala 'a Ngereza 'fasiri Kiswahili; naye 'sema sasa kuwa fasiri 'ake si safi- 'tazuia 'shahara 'ake; na 'ampi ng'oo kazi tena. Takuwa katika taabu kubwa maskini*."(uk.29)

Hapa mwandishi anatueleza kuwa licha ya kuwa mtoto huyu anazungumza lugha ambayo siyo sanifu lakini anataka kutufikishia ujumbe fulani kuwa katika jamii kuna uonevu wa hali juu unaotendeka dhidi ya wanawake. Amemtumia mtoto mdogo kuelezea sifa za Ayubu kuwa ni mtu mwema sana anayefahamika na watu wa rika zote, wadogo kwa wakubwa. Mwandishi pia anataka kutubainishia kuwa katika jamii yetu dhuluma na uonevu vimekithiri kiasi cha kuwagusa watu wa rika na tabaka mbalimbali. Kwa kawaida lugha kama hii katika jamii ya Waswahili tunategemea izungumzwe na watoto wadogo au watu wa mashamba (vijijini) ambao uelewa wao wa Kiswahili upo chini. Huenda pia mwandishi anataka kutueleza kuwa vipo vilugha mbalimbali katika lugha ya Kiswahili.

Matumizi ya vilugha pia yanathibitishwa na mwanamke anayefanya kazi katika jumuiya ya Adili pale alipotembelewa na Yusufu na Sarah. Mwanamke huyu masikini ambaye naye hakuwa anazungumza Kiswahili sanifu kwa sehemu kubwa, amekuwa akiisifu jumuiya hii kwa kule kuthamini watu licha ya uwezo wake mdogo iliyokuwa nayo. Alipoulizwa na Sarah juu ya kazi anayoifanya alisema, *Fanyaga mimi kazi hii kwa jumuia, kibibi, japo haba wajibu ma'ana, wao tupaga sisi kazi 'takapo; kutoga au kutengezaga au kubadili vitu. Na tukirudishaga pesa za kazi hutupaga*......(uk.64)

Hapa mwandishi anazidi kutuonesha matumizi ya vilugha na ujumbe anaotaka tuupate. Hata hivyo tofauti na taarifa tulizozipata hapo juu kuhusu namna wanawake wanavyodhulumiwa haki zao, mwanamke huyu anaonekana kuwa na mtazamo mwema kuhusu jumuiya ya Adili.

Matumizi ya vilugha pia yamebainishwa katika majibizano baina ya bi Kimbaumbau na mla riba. Bi Kimbaumbau baada ya kupata ufadhili toka kwa Zena, alitaka kwenda kukomboa sufuria yake aliyoiweka rahani kwa mla riba, lakini bwana huyu aligoma kufanya hivyo. Hata pale Zuwena alipojaribu kumsihi bwana huyu kufanya hivyo, alijibu kwa jeuri: *"Si kaji 'ako, 'sichana juri, hapana taka 'juvi 'akohapa mimi. Iko karatasi 'angu, umpa haki mimi jana. Odoke, 'ote 'bili. Hapana taka 'taraji 'ako katika kaji 'angu –haya odoke!* (uk.97)
Mwandishi hapa anatuonesha namna watu wenye fedha wanavyowanyasa watu wa hali ya chini ambao mtaji wao unategemea mikopo midogomidogo. Mwandishi ametumia vilugha katika kuonesha tabaka la huyu mla riba. Hata katika jamii yetu ya leo watu wa tabaka hili bado tunao, na unyanyasaji kama huu bado unaendelea. Bado kungali na malalamishi mengi ya unyanyasaji kwa watu wanaofanya kazi mbalimbali masjumbani na kazini mwa watu wengine.

Hata hivyo, ni muhimu tufahamu kuwa kitabu hiki kimeandikwa miaka ya sitini, hivyo yawezekana matumizi ya Kiswahili sanifu hayakuwa yameenea sehemu kubwa ya jamii yetu. Hii inaweza kuwa sababu ya wahusika mbalimbali kutumia Kiswahili ambacho si sanifu na ambacho katika makala hii tumekirejelea kama vilugha. Pamoja na hoja hii, bado ukweli unabaki palepale kuwa matumizi haya ya vilugha ni mchomozo unaobainisha mtindo wa mwandishi huyu kwani angeweza kayaeleza haya aliyoyaeleza kwa Kiswahili Sanifu ukizingatia kuwa hii ni kazi ya nathari.

**Hitimisho**

Makala hii imelenga kufanya uchambuzi wa mtindo kama ulivyotumiwa na Shaaban Robert katika riwaya ya *Siku ya Watenzi Wote*. Mtindo wa mwandishi huyu umebainishwa kwa kuangalia vipengele mbalimbali vya lugha; ambavyo ni matumizi wa uwili, ushairi na vilugha. Vipengele hivi vinaweza kutumika katika kumtofautisha mwandishi huyu na waandishi wengine au kazi hii na kazi nyingine zilizoandikwa na mwandishi huyu ama zile zilizoandikwa na waandishi wengine. Hata hivyo, kwa kuwa mwandishi huyu ameandika kazi nyingi za kifasihi na zisizo za kifasihi, uchambuzi mwingine wa mtindo unaweza kufanywa kwa kuangalia kazi hizo; lengo likiwa ni kuona kama vipengele hivi vya kimtindo vinaweza pia kutofautisha kazi mbalimbali za mwandishi mmoja au la. Kadhalika uchambuzi mwingine unaweza kufanywa kwa kulinganisha kazi mbili tofauti ili kuona namna mtindo unavyoweza kutumika kutofautisha kazi hizo. Suala la kuzingatia hapa ni kuwa katika kufanya uchambuzi wowote wa mtindo, ni muhimu mtazamo au mitazamo itakayotumika iwekwe bayana. Hii ni kutokana na ukweli kuwa kuna mitazamo mingi inayofafanua dhana ya mtindo japo pia mitazamo hii kwa kiasi kikubwa inaingiliana na kukamilishana.

**Marejeo**


Crystal, D. Na Davy, D. (1969). *Investigating English Style*. London: Longmans, Green and Co. Ltd

Enkvist, N. E (1973). *Linguistic Stylistics*. The Hague. Mouton.

Kahigi, K. K. (1997). “Structural and Cohesion Dimensions of Style, A Consideration of some Swahili Texts in Maw (1974)”. *Journal of Linguistics and Language of Education* [New series], Juzuu 3, uk.1-79.

Robert, R. ( 1968 ) *Siku ya Watenzi Wote*, Nairobi: Nelson